
# "HAMASISHA, HAMASISHA, HAMASISHA. JINSI GANI TUNAFANYA!"

*Shiriki mbinu zetu bora zaidi za uhamasishaji barani Afrika.*



FITH · IDWF · FITD

Shirikisho la kimataifa la wafanyakazi wa majumbani

APRILI 19, 2023

...

# Shirikisho la Kimataifa la Wafanyakazi wa Majumbani-IDWF

## *Kuhusu IDWF*

Shirikisho la Kimataifa la Wafanyakazi wa Majumbani (IDWF) ni shirika la wanachama lenye mtandao wa kimataifa wa wafanyakazi wa majumbani. Lengo letu ni kuwaunganisha wafanyakazi wa majumbani ili kupigania haki zao, kuondoa unyonyaji, ukatili, kupata heshima, haki na usalama..

IDWF ilianzishwa mwaka 2013. Miaka kumi baadaye, ilikuwa na vyama shiriki 88 kutoka nchi 68, vikiwakilisha zaidi ya wanachama 670,000.

## *Kuhusu IDWF Kanda ya Afrika*

Kanda ya Afrika, IDWF ina vyama shiriki 28 kutoka nchi 28 zinazozungumza Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Hadi kufikia Februari 2023 ilikuwa inawakilisha wanachama 105,768.

Tunasaidia vyama shiriki kwa kusaidia juhudi zao za kuandikisha wanachama, kujenga uongozi na uwezo wa wanachama, kuunganisha wafanyakazi wa majumbani kutoka ngazi ya jamii hadi kimataifa..



**Hamasisha, hamasisha, hamasisha, Jinsi gani tunafanya**
*Shiriki njia zetu bora Zaidi za uhamasishaji barani.*

*Afrika*

*Imeandikwa na Chris Bonner*

*Imebuniwa 247studios*

*Aprili 2023*

**Shirikisho la Kimataifa la Wafanyakazi wa Majumbani**

*Website: idwfed.org*

*Email: info@idwfed.org*

*Facebook: @IDWFED*

*Twitter: @IDWFED*

# Yaliyomo


01
Uk. 08
AYA YA KWANZA:
**Kuhusu kijarida hiki**

02
Uk. 10
AYA YA PILI:
**Uhamasishaji na Changamoto zake**

03
Uk. 13
AYA YA TATU:
**Kukuza chama chetu: Mpango wa uandikishaji**

04
Uk. 16
AYA YA NNE:
**Kuanzia ngazi ya chini: Mikakati na Mbinu Bora**

05
Uk. 30
AYA YA TANO:
**Kumbukumbu za uhamasishaji na Ustawi endelevu**


"HAMASISHA, HAMASISHA, HAMASISHA JINSI GANI TUNAFANYA!"

06
Uk. 32
SEHEMU YA SITA:
Mafunzo kutokana na uzoefu wetu

07
SEHEMU YA SABA:
Nini kifuate
Uk. 34

08
Hitimisho
Uk. 36

# Shukrani

Tunawashukuru wafanyakazi wa majumbani na waandaaji wote waliochangia katika maandalizi ya kijarida hiki. Licha ya majukumu yenu mengi ya kila siku, mliweza kutenga muda kushiriki katika warsha na mikutano, ambapo mlitoa uzoefu mwingi kuhusu mikakati ya uhamasishaji na uandikishaji ya zamani na ya sasa. Baadhi yenu mlijitolea hata kuaandika hadithi zenu, ambazo zimekuwa nyenzo muhimu kwa tafiti za kesi zilizomo ndani ya kijarida hiki.

Tunatoa shukrani za dhati kwa **Vicky Kanyoka**, Mratibu wa Kanda ya Afrika wa IDWF, pamoja na Maafisa Mipango **Deograsia Vuluwa** na **Essi Kotor**, kwa kuanzisha mradi huu, kuratibu ukusanyaji wa mbinu bora kutoka kwa wanachama wa Afrika, na kuongoza maandalizi ya kijarida hiki hadi kukamilika kwake.

Pia tunamshukuru **Chris Bonner** kutoka **WIEGO** kwa kuandaa na kuandika maudhui ya kijitabu hiki, pamoja na wote waliotoa mchango yao hadi kukamilika kwa toleo la mwisho.

Tunatoa heshima maalum kwa **Myrtle Witbooi**, Rais wetu mpendwa aliyefariki dunia, ambaye kijarida hiki kimetolewa kwa heshima yake. Tumevuna mengi kutoka katika uongozi wake, msaada usiokoma, na msukumo wake wa kipekee.

Urithi wake unaendelea kuishi kwa njia nyingi: katika kumbukumbu zetu, kwenye maandishi na rekodi, kupitia video, mitandao ya kijamii, na zaidi ya yote ndani kabisa ya mioyo yetu.



# Ujumbe Kutoka kwa Marehemu Rais wa IDWF – Myrtle Witbooi

Myrtle Witbooi, Rais wetu mpendwa alifariki dunia tar ehe 16 Januari, 2023. Muda mfupi kabla ya kifo chake alitutumia ujumbe ufuatao kwa lengo la ku wahamasisha na kuwapa motisha wafanyakazi wa majumbani Barani Afrika kuendelea kuhamasisha, ku hamasisha na kuhamasisha. Kijarida hiki kimetolewa kwa heshima yake.

## *Kwa nini ni muhimu sana kuimarisha Chama? Kuhamasisha ndiyo nguvu ya mafanikio*

Unapoanzisha shirika lolote, mafanikio yanatokana na kua ndikisha na kuhamasisha. Wanachama ndiyo hujenga vyama imara. Lakini ili kudumisha nguvu hiyo, tunahitaji kupanga na kupanga kila mara.

Wafan yakazi wahamiaji, wa mijini na vijijini huungana kujenga mshikamano. Vyama imara vinaweza kupam bana na changamoto kubwa, hata zisizotarajiwa kama UVIKO-19.

Afrika imepiga hatua kubwa katika kuandikisha wanachama. Lakini kuandikisha wanachama pekee hakuh akikishi haki. Tunahitaji kuwahifadhi wanachama wetu. Hivyo basi, pamoja na uandikishaji tunahitaji elimu. Kuwaj enga wanachama kimaarifa huwezesha wao pia kuwawezesha wengine.

Ujumbe wetu mkuu ni: **“Pangilia au Ufe kwa Njaa.”**

*-Myrtle Witbooi, Desemba 27,2022*

# VIPUFISHO


| | |
|---|---|
| **ACTRAV** | Kitengo cha shughuli za wafanyakazi- ILO |
| **CHODAWU** | Chama cha wafanyakazi wa Hifadhi,Hoteli, wafanyakazi wa majumbani, Huduma za jamii na ushauri. |
| **CIAWU** | Chama cha Wafanyakazi wa Biashara, Viwanda na Sekta zisizo Rasmi. |
| **IDWF** | Shirikisho la Kimataifa la Wafanyakazi wa Majumbani |
| **ILO** | Shirika la Kazi Duniani |
| **KUDHEIHA** | Chama cha Wafanyakazi wa Majumbani, Hoteli, Taasisi za Elimu, Hospitali na Sekta Zinazohusiana nchini Kenya |
| **MTDWA** | Chama cha Wafanyakazi wa Majumbani cha Mulu Tesfa |
| **NDAWU** | Chama cha Wafanyakazi wa Nyumbani Namibia |
| **SADSAWU** | Chama cha Wafanyakazi wa majumbani na Sekta Zinazohusiana cha Afrika Kusini |
| **SINED** | Shirika la Kitaifa la Wafanyakazi wa majumbani |
| **SYNADOT** | Chama cha Kitaifa cha Wafanyakazi wa majumbani-Togo. |
| **SYNEM-GUINEE** | Chama cha Kitaifa cha Wafanyakazi wa majumbani -Guinea. |
| **SYNEMAG-B** | Chama cha Wafanyakazi wa majumbani na Walinzi cha Burkina Faso. |
| **SYTDTEI.CI** | Chama cha Wafanyakazi wa majumbani na Wafanyakazi wa Sekts Isiyo Rasmi |
| **UN** | Umoja wa Mataifa |
| **WIEGO** | Wanawake katika Ajira Isiyo Rasmi: Utandawazi na Uunganishaji. |
| **ZDAWU** | Chama cha Wafanyakazi wa Majumbani na Sekta shiriki zisizo rasmi- Zimbabwe |

SURA YA

01

# KUHUSU KIJARIDA HIKI

*Katika kijarida hiki tunajifunza mbinu bora ambazo wafanyakazi wa majumbani barani Afrika wamebuni na kuendeleza ili kukuza na kuimarisha vyama vyao vya wafanyakazi. Kijarida hiki kinajikita katika hatua ya awali ya ujenzi wa chama, kuwafikia wafanyakazi wa majumbani, na kuwahamasisha kujiunga na chama hatua inayojulikana kama uandikishaji wa wanachama wapya.*



## *Kwa nini IDWF Afrika imetayarisha kijarida hiki?*

Wakati wa Janga la UVIKO-19, wanachama wa IDWF walitambua kwa undani zaidi thamani ya kuwa sehemu ya vyama vya wafanyakazi jengwa na kuimarishwa. Walichukua uamuzi wa kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza wanachama katika vyama vilivyopo na pia kuhamasisha vyama vipya kujiunga na IDWF.

Lengo la IDWF Afrika ni kupata wanachama wapya 40,000 ifikapo mwaka 2025 (yaani 10,000 kila mwaka kuanzia 2022) pamoja na kuwa na mashirika washiriki manne mapya. Katika warsha ya mtandaoni ya kushirikishana mbinu bora za uandikishaji walikubaliana kuandaa nyenzo kama kijarida hiki ili kusambaza uzoefu wao kwa upana zaidi na kusaidia vyama shiriki viweze kukuza idadi ya wanachama wao.

Kujenga vyama vyetu vya wafanyakazi wa majumbani ndiyo hatua ya kwanza ya kuhakikisha kwamba sauti zetu zinasikika na serikali zetu, waajiri wetu, vyama



vya wafanyakazi, umma na dunia kwa ujumla. Bila kuwaunganisha wafanyakazi wa majumbani katika taasisi za kidemokrasia zinazotegemea wanachama na kuongozwa na wafanyakazi wa majumbani ambao wengi wao ni wanawake, tutaendelea kubaki tumetengwa, huku tukifanya kazi katika kaya binafsi za waajiri wetu.

Tutapata ugumu kusimama na kutoa madai yetu kwa sauti. Tutapambana kutambua na kudai haki zetu au hata tusiwe na ufahamu kuhusu haki zenyewe. Ili kukabiliana na hali hiyo lazima tuhamasishe na kukuza vyama vyetu kwa ajili ya kujenga nguvu ya pamoja.

## *Kijarida hiki ni kwa ajili ya nani?*

Kijarida hiki ni kwa ajili ya viongozi wa wafanyakazi wa majumbani na wahamasishaji katika vyama shiriki vya IDWF. Kinaweza pia kusaidia yeyote anayehamasisha wafanyakazi wa majumbani barani Afrika na kwingineko.

## *Kijarida hiki kinaweza kutumikaje?*

Kupata mawazo kuhusu mbinu za uandikishaji, Kupanga mikakati ya uandikishaji katika Chama chako, Kama ch ombo cha elimu katika warsha na majadiliano ya vikundi.

> “Tutapambana kusimama na kutoa sauti juu ya madai yetu

SURA YA

# Kuhamasisha na Changamoto za Uhamasishaji

# 02




*Kwanini tunahamasisha?*

Wafanyakazi wa majumbani wao peke yao hawana nguvu ya kubadilisha hali yao.

Tunajumuika kuimarisha umoja wetu, mshikamano na nguvu ya pamoja ili tuweze kuboresha hali zetu za kiuchumi na kijamii kupitia uwakilishi na hatua za pamoja.

> Kuhamasisha si tu kuwa na idadi. Ni kuhusu wanachama kujua majukumu yao na kuwajibika kwa chama chao.
>
> *-Vicky Kanyoka, "Ripoti ya Warsha ya Zoom,3 Aprili, 2022"*

## *Uhamasishaji Unahusisha Nini?*

Kuhamasisha ni kuwaleta pamoja wafanyakazi wenye maslahi, changamoto na malengo yanayofanana kwa njia iliyo na mpangilio endelevu.

Kama wafanyakazi wa majumbani, tunaungana kwa sababu kazi zetu na changamoto tunazokutana nazo zinafanana, si tu katika nchi zetu bali pia duniani kote.

Kuhamasisha maana yake ni kuendeleza na kudumisha mifumo ya vyama vya wafanyakazi inayozingatia demokrasia, uongozi kujenga unaowajibika, kuwawezesha na wanachama. Ni kutekeleza shughuli mbalimbali kwa pamoja, na kuwawakilisha wanachama katika mazungumzo na waajiri, serikali, na wadau wengine wenye mamlaka juu ya maisha ya wafanyakazi wa majumbani.Hivyo uhamasisha ni kazi isiyokoma.

## *Uandikishaji ni nini?*

Hii ni hatua ya kwanza na muhimu katika mchakato wa uhamasishaji. Ni mchakato wa kuwavutia wafanyakazi kujiunga na chama cha wafanyakazi yaani, kuwahamasisha na kuwaelimisha wafanyakazi ili wajitokeze na kuwa wanachama wa chama cha wafanyakazi wa majumbani

## *Kwa nini tunahitaji kuandikisha wanachama wapya?*

> Bila wanachama, hakuna chama.
>
> *-Nana Rasmané SYNAMAG/B, Burkina Faso*

Chama cha wafanyakazi hakiwezi kuwepo bila wanachama maana yake ni kwamba chama ni wanachama wenyewe! Kuongeza idadi ya wanachama wetu kunamaanisha kuwa tunakuwa na mwonekano mkubwa zaidi na sauti yenye ushawishi.

Waajiri na serikali huwa na uwezekano mkubwa wa kutusikiliza iwapo wanatambua kuwa tuna msingi imara wa wanachama walio hai na wanaoshiriki kikamilifu.

## *Changamoto kuu katika kuongeza wanachama?*

> Ili kifikia malengo, changamoto ni jambo lisiloepukika lakini kuzishinda ndiko kunakotufikisha kwenye mafanikio.
>
> *-Abebu Molla Hunegnaw, MTDWA, Ethiopia*

Tunakabiliwa na changamoto nyingi katika kukuza vyama vyetu. tunakumbana na vikwazo tunapojaribu kuhamasisha wanachama wapya. tunapambana kuwatunza au kuwabikiza wale ambao tayari wako kwenye chama.

**Changamoito: Wanachama wapya**

- **Vigumu Kuwafikia.** Wafanyakazi wa majumbani wanaishi katika nyumba za waajiri wao. Hatuna uwezo wa kufikia maeneo yao ya kazi" (**Marcelline Douei, SYDTEL. CI, Cote D'Ivoire**) "Baadhi ya waajiri hawaturuhusu kukutana na mfanyakazi wa majumbani." (**Sitope Koto, SYNADOT, Togo**)
- **Hofu.** Wafanyakazi wanaogopa kupoteza kazi ikiwa watajiunga na chama. Wanaogopa kuteswa na mwajiri. Waajiri husema, "nyinyi ni chanzo cha matatizo." **(Toindepi Dhure, ZDAWU, Zimbabwe)**
- **Hakuna pesa.** Mshahara mdogo na "gharama kubwa za maisha inamaanisha kuwa wafanyikazi wa majumbani hawana pesa za ziada. Ni lazima watimize mahitaji yao ya kimsingi kabla ya kuchangia chama." (**Joan Gloria, KUDHEI- HA, Kenya**)
- **Hakuna haja.** Wafanyakazi wa majumbani wanasema kwamba hawahitaji chama. Wanasema, "Mwajiri wangu ni mzuri. Sioni kwa nini nijiunge na chama" **(Toindepi Dhure, ZDAWU, Zimbabwe)** au "Naweza kujisemea mwenyewe kwa bosi wangu. Naweza kujadili. Kwa nini nijiunge na chama?" (**Gloria Kente, SADSAWU, Afrika Kusini**)
- Uelewa mdogo. Wafanyakazi wengi wa majumbani "wana uelewa mdogo juu ya chama" (Debora Mwageni, CHODAWU, Tanzania). "Wengi hawajaenda shule na wanaogopa zaidi" (**Asamaou Bah, SYNEMGUINEE**), na "wengine hawapendi." (**Jo- sephine Zongo, SYNEMAG-B, Burkina Faso**)

- **Changamoto ya lugha.** Kuna lugha nyingi za kienyeji katika nchi zetu. “Katika baadhi ya mikoa ya Namibia kuna kikwazo cha lugha. Hawazungumzi Kiingereza hivyo ni vigumu kueleza kuhusu chama.” (**Frieda Naris, NDAWU, Namibia**)
- **Hali ya kijamii**. “Wengi wanaona aibu kuwaambia watu kuwa wao ni wafanyakazi wa majumbani.” (Sandrine Akaffou, SYTDTEI-CI, Côte D ‘Ivoire)
- **Wafanyakazi Wahamiaji**. “Wafanyakazi wahamiaji wana hofu kwamba tutawaripoti na watarudishwamakwao” (**Gloria Kente, SADSAWU, South Africa).** “Wanaogopa kujiunga kwa sababu hawana nyaraka.” (**Nellie Kahua, NDAWU, Namibia**)
- **Ufinyu wa muda**. “Wafanyakazi wa majumbani hawana muda wa kutosha kutusikiliza, nasi pia hatuna muda wa kutosha kuwaelezea.” (**Aimee De Souza, SYNADOT, Togo**)
- **Ufinyu wa rasilimali**. “Kuna ukosefu wa jinsi au uwezo wa kusafiri kwenda mikoani ambako wafanyakazi bado wanahitaji msaada kutoka kwa chama.” (**Nana Rasmané, SYNAMAG/B, Burkina Faso**)

**Changamoto: Kuwababakisha wanachama**

- **Ajira zisizodumu**. Wafanyakazi wa majumbani mara nyingi hawakai kwa muda mrefu kwenye kazi zao, mfano, “Idadi kubwa ya wafanyakazi wa majumbani mijini hurudi vijijini kupiga kura. Baadaye hawarudi tena.” (**Joan Gloria, KUDHEIHA, Kenya**)
- **Kufukuzwa kazi**. Kiwango cha kufukuzwa kazi ni kikubwa. “Wafanyakazi wengine hufukuzwa isivyo haki na waajiri wao pindi wanapogundua kuwa wamejiunga na chama cha wafanyakazi. “(**Nellie Kahua, NDAWU, Namibia**). Wakati wa COVID-19, wafanyakazi wengi wa majumbani walipoteza kazi zao.
- **Mwenendo wa kusuasua wa kesi**. “Maendeleo ya kesi ni ya polepole. Hii huwavunja moyo. Wafanyakazi wa majumbani hutegemea matokeo ya haraka ya kesi zao.” (**Ruth Khakame, KUDHEI- HA, Kenya**)
- **Kupoteza kesi.** Hatuwezi kushinda kila kesi, lakini “wanatarajia ushinde kesi. Hawapimi hali halisi ya kesi. Wanasema, ‘Nimelipa ada ya uanachama, kwa hiyo lazima nishinde. **“(Gloria Kente, SADSAWU, South Africa)**
- **Tayari wamefukuzwa kazi.** Uanachama ni wa muda mfupi kwa kuwa “wanajiunga na chama wanapokuwa tayari wanakaribia kufukuzwa kazi” **(Toindepi Dhure, ZDAWU, Zimbabwe)**
- **Rasilimali** za kidijitali na uelewa wa teknolojia: Ingawa mambo yanaboreshwa, bado wafanyakazi wengi wa majumbani hawana simu janja, au upatikanaji wake ni mdogo, na si rahisi kwao kuunganishwa katika mtandaoni. Kwa wahamasishaji wa wafanyakazi, “kuna upungufu wa vifaa vya kidijitali kama vile kompyuta mpakato na kompyuta za mezani” **(Ruth Khakame, KUDHEIHA, Kenya)**

Licha ya changamoto hizi, vyama vya wafanyakazi wa majumbani vimeweza kuendeleza mikakati ya uandikishaji na mbinu bora, na vimekua zaidi barani Afrika na duniani kote. Kupitia mapambano ya pamoja, wamepata kutambuliwa kitaifa na kimataifa pamoja na kisheria. Wamepambana na kupata haki katika maeneo memgi ya kazi.

Katika sehemu mbili zinazofuata, tutachambua mikakati na mbinu bora tulizotumia kukabiliana na changamoto za uandikishaji wanachama, ambazo zimeleta mafanikio mengi.

> “Idadi kubwa ya wafanyakazi wa majumbani walioko mijini hurudi vijijini kwenda kupiga kura.

SURA YA **03**

# KUKUZA VYAMA VYETU KUPANGA KUINGIZA WANACHAMA



Tumeungana kama wafanyakazi wa majumbani barani Afrika kupitia IDWF. Hata hivyo, tunatoka katika nchi mbalimbali. Kazini, hali na changamoto zetu zinafanana, lakini lugha zetu, mifumo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na ya kimuundo ni tofauti. Tunaandaa mikakati yetu ya uandikishaji kulingana na kile kinachofanya kazi kwetu. Wakati mwingine tunajaribu mkakati mpya na unafaulu. Wakati mwingine tunajaribu na haileti mafanikio makubwa. Mara nyingi tunahisi tunahitaji mawazo mapya. Kushirikiana kuhusu yale yaliyotufaa kunaweza kuwapa wengine mawazo mapya. Tunaweza kubadilisha mawazo hayo ili yaendane na mazingira yetu.

## *Mikakati ya uandikishaji wanachama*

Kuandikisha wanachama wapya kunapaswa kuwa ni shughuli endelevu, lakini mara nyingi tunapanga kufanya juhudi kubwa na kujiwekea malengo. Kwa maneno mengine, tunakuwa na kampeni au msukumo maalum wa uandikishaji wanachama. Kwa hiyo, kabla hatujakueleza mikakati yetu, hebu tuangalie hatua za msingi za kufuata wakati wa kupanga na kutekeleza kampeni ya uandikishaji au hata kwa shughuli za kawaida za uandikishaji wanachama. Hatua hizi zinaweza kutumika popote ulipo.

| Hatua za Kufuatwa | Mifano |
|---|---|
| Hatuwa ya<br>Kwanza:<br>**Fanya Utafiti** | Wafanyakazi wa majumbani wengi wanafanya kazi au kuishi wapi?<br>Aina gani ya wafanyakazi wa nyumbani (kwa mfano, wanaoishi na waajiri, wahamiaji)?<br>Unaweza kuwapata wapi na kwa njia gani? |
| Hatua ya<br>Pili:<br>**Panga Mkakati wa Jumla** | Nani atafanya nini, lini, na kwa muda gani? Ni nini kinawezekana kufanywa? Kuna fursa zipi? Changamoto zipi?<br>Tunatarajia kufanikisha nini?<br>Rasilimali gani zinahitajika – viongozi, fedha, vifaa? |
| Hatua ya<br>Tatu:<br>**Panga na andaa maelezo kwa uangalifu.** | Nani atafanya nini, lini, na kwa muda gani? Ni rasilimali zipi zilizo tayari?<br>Je, maandalizi kama usafiri, fomu za kujiunga, vyombo vya habari yamefanyika?<br>Tutaripoti vipi na kufuatilia maendeleo? |
| Hatua ya<br>Nne:<br>**Tekeleza na fatilia kwa karibu** | Changamoto ni zipi? Unajifunza nini katika utekelezaji?<br>Kuna jambo linaitaji kubadilishwa?<br>Je mnaripoti kwa wakati? |
| Hatua ya<br>Tano:<br>**Tathmini** | Je, Mlitimiza malengo na matarajio yenu? Kipi kilifanikiwa na kipi hakikufanikiwa?<br>Je, kuna haja ya kubadili mkakati mzima? |

“Wengi wetu hufuata taratibu nzuri za kupanga.

**BOKSI**

# SIMULIZI KUTOKA KENYA

**01**

*Kutambua na kuwafikia wanachama wapya watarajiwa.*

Mimi ni **Ruth Khakame**, Mwenyekiti wa Kitaifa wa Baraza la Wafanyakazi wa Majumbani, na Mwenzangu ni **Joan Gloria**, Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Majumbani, Hoteli, Taasisi za Elimu na Hospitali- Kenya (**KUDHEIHA**). Wote wawili tulichaguliwa kushika nyadhifa hizi. Mpaka Kufikia mwezi Desemba 2022, chama chetu kilikuwa na wanachama wa kazi za majumbani wanaolipia ada za uanachama **12,967**.

Kabla hatujatoka kwenda kuandikisha wanachama wapya, tunaandaa ramani (mapping) ili kubaini mahali wanapopatikana wanachama watarajiwa. Tunafanya zoezi hili kila mwaka. Ramani hii hutusaidia kupanga mipango ya uandikishaji kwa mwaka mzima.

Tunayo orodha ya viongozi wa wafanyakazi wa majumbani katika kila kata. Viongozi hawa hutusaidia kubaini sehemu ambazo wafanyakazi wa majumbani wanafanya kazi. Tunatafuta maeneo makubwa ya makazi (estate) ambapo wafanyakazi wa majumbani wengi hufanya kazi. Hujiuliza, "Je, wanaturuhusu kuingia na kutoka?" kwa sababu baadhi ya maeneo yana ulinzi mkali..

Tunaainisha kila kata na kuangalia usambazaji wa wafanyakazi wa majumbani ili kutambua aina ya wafanyakazi waliopo maeneo tofauti. Wafanyakazi wa majumbani huajiriwa kwa aina mbalimbali kama Wanaoishi na waajiri kwa muda wote, Wanaoenda kazini na kurudi kwa muda wote, Kazi ya kipande au Ajira za kuitwa kwa mahitaji maalum. Wafanyakazi wa kipande huwa na sehemu maalum wanapokaa nje ya nyumba za makazi wakisubiri waajiri wanaoweza kuwataka kwa kazi ya masaa machache.

Wanaotoka nyumbani huanza kazi asubuhi na hurudi nyumbani jioni. Wanaoishi na waajiri hukaa katika nyumba za waajiri wao. Baada ya kubaini maeneo wanapopatikana, wahamasishaji wa chama huenda huko wakiwa na vipeperushi na nyaraka nyingine zitakazosaidia kuwashawishi wafanyakazi wa majumbani kujiunga na chama.

Tunatumia wanachama wa wafanyakazi wa majumbani na viongozi kushawishi wafanyakazi wa majumbani wa kike kujiunga na Chama. Tunaiita njia ya rufaa. Imetusaidia kwa sababu wanajijua wenyewe. Hii ni njia nzuri sababu tunawapa malengo na wao kujihisi kutambuliwan na Chama kwa kile wanachofanya.

**Nellie Kahua, Katibu Mkuu wa NDAWU, Namibia,** anatukumbusha kuandaa vifaa vyetu vya kuandikisha wanachama. "Kabla ya kuanza kuandikisha, hakikisha kuwa vifaa na rasilimali" unazoitaji kwa ajili ya kampeni zinapatikana, kwa mfano, fomu za uandikishaji, vipeperushi na orodha ya namba za simu zilizohakikiwa kwa ajili ya mawasiliano ya badae.

SURA YA

# 04

# KUANZIA MATOKEO MWANZO MZURI: MIPANGO NA MIKAKATI



Mchoro hapo juu unatoa muhtasari wa haraka wa mikakati na mbinu bora t unazotumia kukuza na kuimarisha vyama vyetu. Baadhi ya mikakati hii i nafaa zaidi wakati wa kampeni ya uandikishaji wanachama wapya, ilhali mingine inaweza kutumika katika shughuli za kila siku za kuandikisha w anachama. Pia zipo mbinu zinazosaidia z aidi katika kuwabakisha wanachama wa liopo katika chama. Mbinu nyingi hutumika kwa pamoja, kwa mfano, k utumia zana za mawasiliano ili kuunga m kono shughuli nyingine.

Mbinu zote zilizotajwa hapa zimewahi k ujaribiwa na baadhi ya vyama shiriki v ya Afrika. Kumbuka kwamba chama k inaweza kutumia zaidi ya mkakati mmoja kwa wakati mmoja, au kubadilisha mbinu kulingana na mazingira! Chagua mbinu zile unazrofikiri zinafaa zaidi katika hali yako no ujaribo kuzitumia.

## *Kuwaandikisha wafanyakazi wa majumbani: hadithi zetu.*

Mitaani na kwenye maeneo ya wazi; majumbani na kwenye jamii, viongozi na wahamasishaji hukutana na kuwasiliana na wanachama wapya watarajiwa. Hufanya kazi peke yao, wawili wawili au kwa makundi. Wanazo zana nyingi za zamani na mpya za mawasiliano zinazowasaidia. Wanapata msaada kutoka kwa wanajamii, vyama vya wafanyakazi, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), taasisi za Umoja wa Mataifa (UN), maafisa wa serikali wanaounga mkono juhudi zao, na hata mashirika ya ajira. Kufanya kazi na mashirika ya ajira ni moja ya mikakati inayotumiwa na **SYDTEI-CI kutoka Côte D'Ivoire**.

"Tumekuwa tukifanya kazi kwa muda mrefu na mashirika ya ajira. Tuliwapa elimu kuhusu mazingira ambayo wafanyakazi wa majumbani wanayafanyia kazi. Tuliwaeleza kwamba mara nyingine sheria haiko upande wa wafanyakazi wa majumbani. Tuliwapa vipeperushi kwa ajili ya ofisi zao, na wao huwapa wafanyakazi wa majumbani, wakiwaeleza kuhusu umuhimu wa kujiunga na chama. Leo hii ni washirika wetu. Ni watu muhimu sana kwetu kwa sababu kila siku wanapokea wafanyakazi wa majumbani wanaotafuta ajira." - **Sandrine Akaffou**)

Kwa maneno mengine, wanatumia mikakati mbalimbali, mbinu na zana tofauti kuhamasisha wafanyakazi wa majumbani kujiunga na chama na pia kuendeleza uanachama wao.

> Njia zetu za zamani bado muhimu sana.
>
> *- Joan Gloria, KUDHEIHA, Kenya*

## 1. Maeneo, Nafasi na Watu

Mbinu za zamani za kuandikisha wanachama wapya, hasa kwa njia ya ana kwa ana, bado zina umuhimu mkubwa. Wakati wa janga la UVIKO-19 tulijifunza kutumia teknolojia mpya kwa ufanisi zaidi, na tumekuwa tukizijumuisha katika mbinu zetu za kazi. Hata hivyo, teknolojia haijachukua nafasi ya mbinu za zamani tulizozijaribu na kuthibitisha ufanisi wake. Kilichobainika ni kwamba kukutana ana kwa ana na wafanyakazi wa majumbani bado ni njia bora kabisa ya kuwashawishi kujiunga na chama. Kama alivyonukuliwa **Gloria Kente** kutoka **SADSAWU, Afrika Kusini**, "Kukutana ana kwa ana ni vizuri. Wanapotuona, hujihisi kuwa matatizo yao yote yatapata suluhisho." **Vicky Kanyoka**, Mratibu wa Kanda wa IDWF, aliongeza kuhusu manufaa ya kisaikolojia, "Mikutano ya ana kwa ana ni muhimu sana katika kusaidia kuponya majeraha yao. Wafanyakazi wa majumbani wengi wana majeraha ya kihisia, hivyo kukutana nao ni kama ushauri nasaha na wanapata nafasi ya kueleza matatizo yao."

### Nyumba kwa Nyumba: Mahala pa kazi

"Tunapohamasisha, huangalia maeneo yenye idadi kubwa ya wafanyakazi wa majumbani. Tunaenda nyumba kwa nyumba. Tunapiga hodi na kuuliza kama kuna mfanyakazi wa majumbani hapa. Tunazungumza nao kuhusu chama cha wafanyakazi. Tunaenda wawili wawili ili tuweze kuzungumza nao kwa Kifaransa au kwa lugha yao ya asili. Kuwazungumzisha kwa lugha yao ni jambo muhimu sana." (**Aimee de Souza, SYNADOT, Togo**)

Vyama vya wafanyakazi vinatumia mbinu hii ya kwenda nyumba kwa nyumba: kuwafikia wafanyakazi wa majumbani katika nyumba za waajiri wao hasa wale wanaoishi kwa waajiri na pia kuwafikia katika makazi yao binafsi baada ya kazi au siku za mwisho wa wiki kwa wale wanaorudi nyumbani kila siku. Ingawa ni changamoto kuwafikia wafanyakazi wa majumbani katika nyumba za waajiri wao, viongozi wa wafanyakazi wa majumbani katika maeneo husika hujuana, na pia hujua mahali ambapo kuna wanachama wapya watarajiwa. Hufanya ziara mchana wakati mwajiri akiwa kazini. Watapiga hodi, na mfanyakazi wa majumbani atatoka nje. Wataonesha bango au kipeperushi na kuzungumza naye kuhusu chama cha wafanyakazi. Kisha humwachia namba ya simu ili baadaye aweze kupiga simu kwa maelezo zaidi au kujiunga na chama. Katika baadhi ya matukio, walinzi wa nyumba wamekuwa msaada mkubwa katika kuwaunganisha viongozi wa vyama na wafanyakazi wa majumbani waliopo ndani ya nyumba hizo. Kuna mbinu moja ya kipekee lakini huenda ikazua mjadala inayotumiwa na CHODAWU, Tanzania ambapo,

"Tunachukuwa kiongozi mmoja wa wafanyakazi wa majumbani pamoja na Afisa mmoja

wa serikali ya mtaa kwa sababu wao wanajua mahali wafanyakazi wa majumbani walipo. Tunaenda nyumba kwa nyumba pamoja na Maafisa hao kwa ajili ya kuandikisha wanachama. Tuna uhusiano mzuri na Maafisa wa Serikali na tumewapa mafunzo kuhusu hali halisi ya wafanyakazi wa majumbani na thamani yao." (**Debora Mwageni, CHODAWU, Tanzania**)

## Mlango kwa Mlango: ndani ya jamii

Kuandikisha wanachama kwa kwenda mlango kwa mlango pia hufanyika ndani ya jamii kwa ajili ya wafanyakazi wa majumbani wanaoishi kwa waajiri. **Nellie Kahua** kutoka **NDAWU, Namibia**, anaeleza faida za mbinu hii.

"Kuenda nyumba kwa nyumba katika jamii kuna unafuu zaidi kwa wafanyakazi wa majumbani. Unawakuta wakiwa katika mazingira yao ya nyumbani na wakiwa na utulivu. Wakati anapofanya kazi za nyumbani kama kupika, tunajitambulisha na kueleza historia ya chama. Pia, anaweza kuwa na hofu ya kwenda ofisini. Akiwa nyumbani, hahitaji kutumia rasilimali zake ndogo kuhudhuria kikao au kwenda ofisini. Kisha yeye mwenyewe huwashawishi marafiki zake na majirani kujiunga."

**CIAWU** nchini **Malawi** inatumia mbinu kama hiyo:

"Tunaingia majumbani kukutana na wafanyakazi wa majumbani na kujitambulisha. Tunawaeleza kuhusu chama cha wafanyakazi, jinsi kinavyofanya kazi, Jinsi wanavyoweza kujiunga na kujua haki zao mahala pa kazi. Wanapojiandikisha kwa kujaza fomu inayogharimu MK 200, wanakuwa wanachama na wanashauriwa kulipa ada ya uanachama ya 1% kila mwezi." (Peter Chaunga, CIAWU, Malawi)

Hadithi hii pia inaibua suala la ada za chama na jinsi bora ya kuwaeleza wafanyakazi wa majumbani ambao kipato chao ni kidogo. Ni muhimu kueleza lengo la ada ya chama, na kwamba ni ishara ya kujitoa kwa chama. Pia ni muhimu kueleza kiwango kinachopaswa kulipwa kwa uwazi.

"Tunawaambia kuwa ada ya uanachama ni ndogo — la sivyo hawataki kujiunga," Anasema As- maou Bah (SINEM-GUINEE)

## Maeneo na nafasi: Karibu na mahala pa kazi

Kuna maeneo mengi ambayo wafanyakazi wa majumbani hupita kwenda kazini, au Hukusanyika karibu na maeneo yao ya kazi. Haya ni maeneo mazuri yanayowapa viongozi fursa ya kuzungumza nao kuhusu chama cha wafanyakazi.

Viongozi wengi wa wafanyakazi wa majumbani ni au waliwahi kuwa wafanyakazi wa majumbani wenyewe. Wanajua mitaa na njia ambazo wafanyakazi wa majumbani hutumia kwenda na kurudi kutoka kazini. Wanajua vituo vya mabusi na teksi wanavyotumia kupanda au kushuka. Viongozi huamka mapema asubuhi na kwenda katika maeneo haya kukutana na wafanyakazi wa majumbani.Wanabeba mabango, vipeperushi na stika, katiba ya chama, fomu za usajili huku wakiwa wamevaa mashati na kofia za chama ili wafanyakazi wa nyumbani waweze kuwatambua. Wafanyakazi wa majumbani wenyewe njiani kwenda na kutoka kazini pia husaida kwa kuzungumza na wenzake juu ya umoja.

Kuna maeneo karibu na sehemu wanapofanyia kazi wafanyakazi wa majumbani ambayo ni fursa nzuri kwa viongozi hukutana nao mitaani kwenye bustani wanapokuwa wakisukuma magari ya watoto, pembezoni mwa barabara ambapo wafanyakazi wanaoishi na waajiri hukusanyika kuzungumza baada ya kazi; au sehemu ambapo wafanyakazi wa kazi za vipande au wa vijiweni husubiri kutafuta kazi. Katika maeneo haya, viongozi hukutana na wafanyakazi wakiwa na vifaa vyao vya kampeni na mavazi ya Chama ili kuwahamasisha wajiunge na chama. Huwapa vipeperushi vyenye mawasiliano kama vile namba za simu, ujumbe mfupi au WhatsApp, au anwani ya ofisi ili wapate taarifa zaidi au kujiunga. Laura Tembe Manhiça kutoka SINED, Msumbiji, anaelezea ratiba yake ya asubuhi:

"Nafanya kazi hii ya uandikishaji siku tatu kwa wiki, Jumatatu, Jumatano na Ijumaa. Katika

siku hizo, huamka saa 10:00 alfajiri, naosha vyombo, kufagia uwanja, kuoga na kujiandaa kwa kazi (kupanga nguo, aproni), vifaa vya kampeni (fulana, stika, vipeperushi). Saa 11:25 napanda basi la kwanza kutoka Kituo cha Socimol kuelekea katikati ya jiji.

Kwa kawaida hufika mjini saa 12:10 asubuhi na ifikapo saa 12:20 huenda kukutana na viongozi wengine wa chama. Baada ya kukutana kwenye uwanja wa wafanyakazi (eneo la mkutano), tunagawana vifaa vya kampeni na kugawanyika kwa mujibu wa mitaa, kisha mimi huanza kazi ya kuhamasisha na kuandikisha wanachama."

*Maeneo na nafasi: Ndani ya jamii*

Wafanyakazi wa majumbani wanaoenda na kurudi ni sehemu ya jamii wanamoishi na mara nyingi ni wanachama wa mitandao mbalimbali ya kijamii. Wanatumia mitandao hiyo kujiandaa, kujipanga na pia kuwapa taarifa viongozi wa chama kuhusu maeneo wanamoishi au wanapopatikana mara kwa mara wafanyakazi wa majumbani. Baadhi ya maeneo mazuri ya kuwaandikisha wanachama wapya ni kwenye mikusanyiko ya kidini, masoko na supermarket ambako wafanyakazi wa majumbani huenda kununua mahitaji, pamoja na mikutano ya kijamii.

"Masokoni, makanisani popote tunapowaona tunazungumza nao kuhusu chama. Hatupendi kukaa ofisini. Tunatoka na kwenda kuwafikia." **(Aimee de Souza, SYNADOT, Togo)**

Jambo muhimu lililosisitizwa na viongozi wengi ni kwamba wafanyakazi wa majumbani wenyewe ndiyo wahamasishaji bora zaidi wa wenzao.

> Wafanyakazi wa Majumbani hujihamasisha vyema zaidi wao wenyewe. Wanajua sehemu ambapo wafanyakazi wengine wa majumbani walipo na wanaweza kuwasiliana nao vyema.
>
> *- Ruth Khakame, KUDHEIHA, Kenya*

BOKSI

02

# MASWALI KUTOKA KWA WAFANYAKAZI WA MAJUMBANI

*Jinsi ya kujibu maswali ya wafanyakazi wa majumbani*

Ruth Khakame na Joan Gloria (KUDHEIHA, Kenya) pamoja na Abebu Molla Hunegnaw (MDWA, Ethiopia) wamebainisha baadhi ya maswali magumu ambayo wahamasishaji huulizwa na wafanyakazi wa majumbani wakati wa kampeni za kujiunga na vyama. Hapa pia walitoa majibu yanayosaidia kufafanua masuala hayo.

**Kenya**

- Chama ni nini? Je, ni chama cha akiba?
- Je, nitarudishiwa pesa zangu nikiacha kuwa mwanachama?
- Nitafaidika vipi nikijiunga na chama?
- Ofisi zenu ziko wapi?

Tunawaeleza kuwa chama sio chama cha  kuweka akiba na ada ya uanachama inalipwa kama ada ya huduma na haitorudishwa ni kama kuchangia mfuko wa bima ya afya ya NHIF ukikosa kuugua hupati marejesho. Ili kuwaondoa wasiwasi tunawambia wahudhurie mikutano ya wanachama kila mwezi ili waelewe Zaidi kuhusu faida za kuwa mwanachama wa chama cha wafanyakazi wa majumbani.

**Ethiopia**

- Je, kuna faida gani kuwa mwanachama wa chama cha wafanyakazi wa majumbani?
- Je, chama kinatulipa au kutupatia fedha?
- Chama kitasaidiaje kutetea haki zetu?
- Je, chama kinaweza kutupatia kazi?
- Je, chama kinatoa mafunzo ya aina gani?

Tunafafanua kuwa Chama ni taasisi ambayo:

- Tunasaidiwa kutetea haki zetu za kijamii na kiuchumi
- Tunabadilishana uzoefu mzuri na wenzetu
- Tunajenga uwezo wetu wa mawasiliano
- Tunajadiliana changamoto tunazokutana nazo kazini na kutafuta suluhisho
- Tunapewa mafunzo kuhusu sheria na miongozo ya kazi
- Tunapata mafunzo ya stadi za maisha na shughuli za kujipatia kipato

*Katika matukio ya umma*

Siku ya wafanyakazi Duniani (Mei 1), Siku ya Wafanyakazi wa Majumbani Duniani (16 Juni), Sik u ya Wanawake Duniani (8 Machi), utawaona wafanyakazi wa majumbani wakiwa mitaani wakiwa wamevaa fulana za chama, wakiwa na mabango, wakiimba nyimbo za mshikamano na kuelimisha kuhusu chama chao. Mara nyingi hushiriki maandamano au mikusanyiko na wafanyakazi wengine au wanajamii. Pia hushiriki katika shughuli za kijamii kama vile upandaji miti, kama ilivyofanyika Kenya ambapo wafanyakazi wa   majumbani walishiriki katika tukio la upandaji miti. Shughuli hizi zote hutoa elimu na hamasa kwa wafanyakazi wa majumbani kwamba wao ni wafanyakazi halali kama wengine, na kuwa chama ni chao. Hii huwatia moyo na kuwahamasisha kujiunga na chama.

Taarifa na picha za matukio haya husambazwa kwa wanachama na kwa jamii kwa upana zaidi kupitia mitandao pamoja na vyombo vya habari kama vile redio na magazeti. Lengo kuu ni kuongeza uelewa kuhusu hali halisi ya wafanyakazi wa majumbani miongoni mwa wafanyakazi wengine, wanajamii na umma kwa ujumla.

Tumebaini kuwa kuwaandikisha wafanyakazi wa majumbani wahamiaji ni changamoto kubwa. Nchini Afrika Kusini, SADSAWU imekabiliana na changamoto hii kwa kuandaa mkakati madhubuti wa kuwaandikisha wafanyakazi wa majumbani wahamiaji. **Gloria Kente** anasimulia jinsi walivyofanikisha jambo hili.

BOKSI 03

## HADITHI KUTOKA AFRIKA KUSINI

*“Wanaelewana wenyewe” Mkakati wangu wa kuandikisha wafanyakazi wa majumbani wahamiaji.*

Jina langu ni **Nomasomi Gloria Kente**. Mimi ni raia wa Afrika Kusini na mratibu wa chama cha wafanyakazi kiitwacho **South African Domestic, Service and Allied Workers Union (SADSAWU)** ambacho kina takriban wanachama 9,000.

Mkakati wangu wa kuandikisha wafanyakazi wahamiaji ni kuwaalika wahamiaji ambao tayari ni wanachama wa SADSAWU kujiunga nami katika shughuli za uandikishaji.

Naenda pamoja nao kuwafikia wahamiaji wengine kwa sababu wao ndiyo wanaoathirika zaidi na unyonyaji hapa Afrika Kusini. Kuwachukua wanachama wahamiaji waliopo kunasaidia sana, kwa sababu wanaweza kuwaelewa wenzao vizuri na kuwahamasisha kujiunga na chama.

Mkakati huu umezaa matunda, kwani wahamiaji wengi wamejiunga na SADSAWU baada ya kuelewa chama hiki ni nini na kwa nini wanapaswa kuwa wanachama wake.

Bila shaka nilikumbana na changamoto baadhi ya wafanyakazi waliona hakuna haja ya kujiunga kwa sababu waliamini waajiri wao hawatawadhulumu. Wengine walikuwa na hofu kuwa SADSAWU ingewaripoti kwa Idara ya Uhamiaji na wangefukuzwa nchini.

Nilikabiliana na changamoto hizi kwa kutoa elimu kwa wafanyakazi wa majumbani kuhusu SADSAWU na kwa kufanya kampeni kubwa za uandikishaji kila mwisho wa wiki.

Nilifuatilia kwa kuwasiliana na wanachama kupitia mitandao ya kijamii, simu na ujumbe mfupi wa maandishi (SMS).

Haikuwa rahisi kushughulika na watu nisiowajua, lakini nilichojifunza ni kwamba unapaswa kuelewa watu wanatoka wapi na ujifikirie ungekuwa kwenye nafasi yao ili uweze kushirikiana nao kwa ufanisi.

## 2. Shughuli za uwezeshaji wa pamoja.

*Mikutano ya kuongeza*

Baada ya mawasiliano ya awali na wafanyakazi wa majumbani wapya au wanaotarajiwa kujiunga na chama, vyama vingi huwaalika kushiriki katika mikutano ya kuongeza uelewa.

Mikutano hii inaweza kuwa maalum kwa ajili ya wanachama wapya au wanaotarajiwa, au wanaweza kuunganishwa katika mikutano ya kawaida ya kila mwezi.

"Tunakutana na wanachama wetu kila mwezi kusikiliza matatizo yao na kuwasaidia. Tunakaribisha wafanyakazi wapya kuja. Wanasikiliza na kisha huwa tayari kuchukua kadi zao za uanachama." **(Josephine Zongo, SY-NAMED/B, Burkina Faso)**

Mikutano hii ni muhimu sana katika kujenga imani na ujasiri kwa chama. Katika mikutano hii, viongozi huweka wazi maana ya chama, Malengo yake na jinsi kinavyofanya kazi. Pia huwaeleza umuhimu wa kujiunga na chama na faida za kuwa mwanachama. Pia huwasilisha haki za wafanyakazi wa majumbani chini ya sheria na namna chama kinavyowasaidia kupigania haki hizo. Hutoa mifano ya kesi walizoshinda lakini huweka wazi kuwa ni mapambano ya pamoja na sio matatizo yote yanaweza kutatuliwa mara moja. Katika baadhi ya mikutano, viongozi huwatambulisha wanachama wapya kwa Shirikisho la Kimataifa la Wafanyakazi wa Majumbani (IDWF). Hili husaidia kuongeza uhalali wa chama na kuwaelimisha wafanyakazi kuhusu harakati za kimataifa.

"Tunawaeleza kuhusu IDWF na tunawaomba watembelee tovuti ya IDWF ili waone shughuli mbalimbali. Huuliza, 'je, tunaweza kweli kuwa na chama cha kimataifa?' Hii huongeza imani yao." (Marecelline Douai, SYTD- TEI-CI, Côte d'Ivoire)

*Uimbaji huchochea hamasa*

Nyimbo na ngoma, kauli mbiu na ushuhuda vina mchango mkubwa katika mikutano mingi ya wafanyakazi wa majumbani. SADSAWU ina kikundi chake cha kwaya ya wafanyakazi wa majumbani ambacho huimba katika mikutano na matukio mbalimbali ya chama.

"Nyimbo hutumika kuelezea hisia zetu za huzuni, furaha, msukumo! Tunaimba tunapokusanyika. Tunatuma ujumbe kupitia nyimbo zetu. Nyimbo hizi hurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi na hubeba ujumbe wa kihistoria kuhusu mapambano ya zamani. Nyimbo huathiriwa na tamaduni za Kiafrika za wafanyakazi na tabaka la wafanyakazi kama nguvu maalum. Ni njia ya mawasiliano na njia ya kujenga mshikamano." **(Toindepi Dhure, ZDAWU, Zimbabwe)**

Baada ya mikutano, wakiwa wamesisimka na nyimbo zenye ujumbe mzuri na ngoma za kufurahisha, wale ambao bado hawajajiunga na chama hujaza fomu na kujiunga rasmi.

### BOKSI 04

### MASWALI KUTOKA KWA WAFANYAKAZI WA MAJUMBANI

*Wimbo pendwa wa wafanyakazi wa majumba*

Mama yangu ni msichana wa jikoni,
Baba yangu ni mvulana wa bustani
Ndio maana mimi ni mfuasi wa vyama vya wafanyakazi.
Ndio maana mimi ni mfuasi wa vyama vya wafanyakazi,
Ndio maana mimi ni mfuasi wa vyama vya wafanyakazi,
Mimi ni mfuasi wa vyama vya wafanyakazi.

*Kutoa mafunzo*

Vyama vyetu vya wafanyakazi hutoa mafunzo na shughuli za kujenga uwezo kwa wanachama wapya pamoja na wale waliopo kwa muda mrefu, kwa lengo la kuwawezesha kama wanachama na kama wafanyakazi. Mafunzo endelevu, warsha na matukio mbalimbali ni muhimu sana kwa kuendeleza hamasa, ushiriki na uhai wa wanachama ndani ya chama. Ikiwa vyama havitashughulikia masuala yanayowahusu wanachama, havitaendesha kampeni za uhamasishaji, warsha, au kutoa fursa za mafunzo, basi wanachama hawataona sababu ya kubaki ndani ya chama. Nchini Ethiopia, MTDWA hutoa mafunzo kuhusu sheria na sera za kazi pamoja na mafunzo ya ufundi na shughuli za kujiongezea kipato. Nchini Afrika Kusini, chama cha SADSAWU huendesha mafunzo juu ya ujuzi wa uongozi, stadi za kidijitali, na kazi za mikono, miongoni mwa mengine.

## 3.Kuandaa harakati ili kulenga masuala ya wafanyakazi wa majumbani

*Kutatua matatizo na kutoa huduma*

"Ni muhimu sana kushughulikia masuala na madai ya wafanyakazi wa majumbani kwa uhalisia na uwajibikaji. "Usiwe mtu wa maneno tu; wasikilize, zungumza nao na tafuteni suluhisho pamoja." **(Toindepi Dhoure, ZDAWU, Zimbabwe)**

Moja ya matarajio makubwa ya wafanyakazi wa majumbani ni kuona kuwa viongozi na wahamasishaji wa chama wanashughulikia malalamiko yao kwa dhati na kuwasikiliza. Iwapo viongozi wa chama ni waaminifu, wa wazi, na wanapatikana kwa urahisi kwa wanachama, basi wanachama wataendelea kufika ofisini wakiwaletea kesi na changamoto zao za kikazi.

Pale ambapo viongozi hutoa huduma bora kwa kufuatilia kesi, kuzitatua kwa ufanisi, na kutoa ushauri mzuri wanachama huwaeleza wafanyakazi wenzao ambao nao hukumbwa na matatizo kazini. Hii huleta imani na kuvutia wanachama wapya wengi kujiunga

"Mkakati wa kwanza unajikita katika kutatua migogoro ya kazi kupitia mahakama; wafanyakazi wanaoridhika na upatanisho au uamuzi wa kesi hueneza taarifa kwa wenzao wasio wanachama, ambao nao huamua kujiunga na chama." **(Nana Rasmané, SYNEMAG/B, Burkina Faso)**

Uzoefu wa vyama wakati wa janga la UVIKO-19 umeonyesha kwa uwazi umuhimu mkubwa wa kushughulikia mahitaji ya dharura ya wafanyakazi wa majumbani, na jinsi hiyo ilivyosaidia kujenga nguvu ya vyama. Vyama vingi viliripoti kuwa vilipata ongezeko la wanachama wakati wa janga hilo, kwa sababu vilitoa msaada wa moja kwa moja kwa wafanyakazi wa majumbani waliokuwa wakikabiliwa na msongo wa mawazo na matatizo ya kiafya na kiuchumi. **Sitopi Koto kutoka SYNADOT, Togo,** anakumbuka tukio hilo:

"Tulipata wanachama wapya 600 wakati wa UVIKO.19 Tuligawa chakula kwa watu baada ya kupokea msaada kutoka kwa IDWF. Watu walikuwa wakiuliza, 'Huyu anayegawa chakula ni nani? Ni serikali?' Tulichukua muda kuwaeleza kuhusu chama na kuhusu IDWF "

**Asmaou Bah,** kutoka SYNEM-GUINEE naye anatoa uzoefu kama huo:

"Tulitumia UVIKO-19 kama fursa ya kupata wanachama wapya. Kabla ya UVIKO-19 tulikuwa na wanachama 2,000. Sasa tuna wanachama 3,000 kwa sababu ya msaada tuliowapa wafanyakazi wa majumbani."

*Kampeni za utetezi kuhusu madai muhimu*

Kuendesha kampeni za utetezi kuhusu madai na changamoto kubwa zinazowakabili wafanyakazi wa majumbani katika nchi zao kama vile ulinzi wa kijamii au kuhusu masuala makubwa ya kimataifa kama kuridhia na kutekeleza Mkataba wa ILO Na. 189 (C189), huchangia sana kuongeza uelewa kuhusu hali halisi ya wafanyakazi wa majumbani. Kampeni hizi huwalenga viongozi wa serikali na waajiri, lakini pia huwafikia moja kwa moja wafanyakazi wa majumbani na kuwavutia kujiunga na chama kupitia mikakati mizuri ya mawasiliano. Uungwaji mkono kutoka kwa washirika kama vile mashirikisho ya vyama vya wafanyakazi ya nchi, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), na mashirika ya kimataifa kama ILO huweza kuimarisha zaidi kampeni hizi.

**Asmaou Bah** kutoka SYNEM-GUINEE anaelezea jinsi kudai haki za wafanyakazi wa majumbani kupitia kampeni ya kushinikiza kuridhia Mkataba namba 189 kulivyowezesha kuanzishwa kwa chama mwaka 2011 na kuchangia kukua kwake hadi kuwa shirika lenye nguvu.

BOKSI

# 05

## HADITHI KUTOKA GUINEA

*Kuhamasisha juu ya Mkataba Na.189*

Mimi ni Asmaou Bah, Katibu Mkuu wa Chama cha Kitaifa cha Wafanyakazi wa Majumbani wa Guinea (SYNEM-GUINEE). Chama chetu kilianzishwa mwezi Machi 2011, mara baada ya mkutano wa maandalizi uliofanyika Johannesburg kuhusu kuridhiawa kwa Mkataba wa ILO Na. 189 (C189) katika Mkutano wa 100 wa Kimataifa wa Kazi uliofanyika Geneva, Juni 2011.

Baada ya kuchaguliwa kwa viongozi wa chama, tulianza kuwafikia wafanyakazi wa majumbani kwa kwenda nyumba kwa nyumba, kwa kusambaza taarifa kwa mdomo, kutembelea nyumba zao, na hata kuwasubiri walipokuwa wakitoka au kuingia kazini. Tulieleza kuhusu Mkataba wa ILO namba 189 unaowalinda, tuliwahamasisha kujiunga na chama, tukiwasajili na kuwapa kadi za uanachama.

Tulisambaza ujumbe kuhusu mkataba namba 189 kwa njia mbalimbali kama Mikutano na waandishi wa habari, Mikutano ya hadhara, Mabango na matangazo.

Redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii kama Facebook na mengineyo. Tuliandaa warsha na mafunzo, tukahakikisha ujumbe unawafikia wafanyakazi wote wa majumbani, hasa walioko vijijini, kwa kutumia lugha za asili.

Shughuli hizi zote zilituwezesha kuwaandikisha wafanyakazi wengi wa majumbani, kuwajengea uwezo, kuwapa uelewa, na hatimaye kujiunga na chama kwa wingi. Matokeo yake ni kwamba SYNEM-GUINEE imekuwa moja ya vyama vilivyojipanga vizuri zaidi ndani ya IDWF. Na kutokana na juhudi za chama chetu, nchi ya Guinea imeridhia rasmi Mkataba wa ILO namba 189 – unaolinda na kutambua haki za wafanyakazi wa majumbani

Sandrine Akaffou kutoka SYTDTEI.CI, Côte D'Ivoire anasimulia taarifa kuhusu kampeni ya ulinzi wa kijamii ya chama chao, ambayo iliendeshwa kwa ushirikiano na mashirika ya Umoja wa Mataifa nchini Côte D'Ivoire, chini ya uratibu wa ILO-ACTRAV.

Hii inaonesha umuhimu wa kushirikiana na vyama vya wafanyakazi pamoja na mashirika ya kimataifa yenye ushawishi na yanayounga mkono haki za wafanyakazi wa majumbani. Mashirika haya yana uwezo wa kukuza kampeni, kufungua milango ya mawasiliano na serikali na taasisi mbalimbali, na pia kukipa chama hadhi na uhalali mbele ya wafanyakazi wa majumbani na jamii kwa ujumla.

> Moja ya matarajio makubwa ya wafanyakazi wa najumbani ni kwamba viongozi washughulikie malalamiko yao na kuyatekeleza madai yao kwa ufanisi.

BOKSI

## 06

# HADITHI KUTO KA CÔTE D'IVOIRE

*Ushirikiano na mashirika ya umoja wa Mataifa*
*Kampeni ya ulinzi wa kijamii kwa wafanyakazi wa majumbani*

Mimi ni Sandrine Akaffou, Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Majumbani na Wafanyakazi wa Sekta Isiyo Rasmi wa Côte D'Ivoire (SYTDTEI.CI).

Tangu mwaka 2019, tumekuwa na mradi wa Kazi za staha kwa Wafanyakazi wa Majumbani kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa, hususan kupitia ACTRAV — Kitengo cha Shughuli za Wafanyakazi katika Shirika la Kazi Duniani (ILO). Ulinzi wa kijamii, ukiwemo bima ya afya kwa wote, ni suala muhimu sana kwa wafanyakazi wa majumbani. Tumekuwa tukifanya kampeni ya kuwahamasisha waajiri wawaandikishe wafanyakazi wao wa majumbani katika mfumo wa hifadhi ya jamii nchini Côte D'Ivoire, kwa kushirikiana na ILO.

Kattia Paredes Moreno, Mtaalamu wa Shughuli za Wafanyakazi wa ILO katika Ofisi ya Kazi ya Kimataifa (ILO) mjini Abidjan, anasisitiza umuhimu wa wafanyakazi wa majumbani kufaidika na haki zao.

Wakati wa maadhimisho ya miaka 77 ya Umoja wa Mataifa (3 Novemba 2022), alinukuliwa akisema,

"Leo nchini Côte d'Ivoire, ni muhimu kwa wafanyakazi wa majumbani kufaidika na haki zao kwa mujibu wa mfumo wa kisheria. Ni suala la kuhakikisha namna bora ya kuwaingiza katika mchakato wa ulinzi wa kijamii, kupitia taasisi ya CNAM (Taasisi ya Hifadhi ya Jamii) na Mfuko wa Kitaifa wa Hifadhi ya Jamii (CNPS)."

Katibu Mkuu wetu, Marceline Douai, alieleza kuwa, "Ulinzi wa kijamii unaojumuisha usalama wa jamii na afya na usalama mahali pa kazi ulitumika kama nyenzo muhimu ya kuwahamasisha wafanyakazi wa majumbani kujiunga na chama na kuwasilisha madai madhubuti kwa serikali. Masuala haya yaliwavutia wafanyakazi wengi kujiunga na chama."

### 4. Zana zetu: Vyombo vya habari vya "kiasili"

*Vifaa vya Elimu*

Katika kila hadithi ya uandikishaji wanachama, tunaona jukumu muhimu linalofanywa na usambazaji na ugawaji wa vifaa vya elimu na utetezi. Vyama vimetengeneza aina mbalimbali ya zana hizo kwa lengo la kuelimisha na kuhamasisha. Baadhi ya zana hizo ni; Vipeperushi, Mabango, stika, Fulana za chama.

Zana hizi ubeba taarifa kuhusu chama na malengo yake, madai ya kazi zenye staha haki za wafanyakazi wa majumbani, mchakato wa kurithia na kutekeleza makataba namba 189, Ulinzi wa kijamii, Ongezeko la mishahara, kauli mbiu za kuhamasisha na mengineyo. Pia chama kimetengeneza na kutumia video za elimu kuhusu chama ambazo uoneshwa katika mikutano ili kusaidia kueleza kuhusu kazi za chama na kushirikisha wanachama wapya au waliopo.

*Redio na Televisheni*

Hizi ni nyezo zenye nguvu sana k atika kuhamasisha wafanyakazi w a majumbani. Viongozi wa vy ama huwafata wahariri au w akurugenzi wa vyombo vya h abari ili kupata muda wa kurusha vipindi vya redio au Televisheni. SYNEHM kutoka Guinea na CHODAWU kutoka Tanzania v ilitumia redio na televisheni kwa ki wango kikubwa katika kampeni y ao ya kuhamasisha kuridhia Mk ataba wa ILO namba 1899. kwa ku wa SADSAWU nchini Afrika Ku sini ni chama kinachotambulika sana, redio mbalimbali huwaita mara kwa mara ili kuwaelezea w ananchi kuhusu vyama vya w afanyakazi na sheria mpya zin azowahusu wafanyakazi wa majumbani.

Vip indi hivi mara nyingi hurushwa mapema asubuhi wakati waajiri wa k iwa kazini na wafanyakazi wa majumbani wakiwa ndani peke yao . Hii huwapa nafasi ya kusikiliza au kutizama jambo am balo huwavutia na kuhamasika kujiunga na chama.

"Tuna nafasi ya bure kwenye televisheni ya taifa. Tunapiga simu tu na kupangiwa kipindi. Tunafanya hivi kabla ya saa 11:45 alfajiri. kipindi hiki ni sehemu ya Good morning Namibia, tunazungumza kuhusu chama chetu" **(Nellie Kahua, NDAWU, Na mibia)**

## 5. Zana zetu: Teknolojia Mpya

*Matumizi ya simu*

Simu za mkononi zimekua zikitumika kwa miaka mingi katika haraki za uandikishaji wa wanachama. Viongozi huwapa wafanyakazi wa majumbani namba zao ili waweze kuwasiliana nao kwa urahisi. Kwa sasa, ujio wa simu janja umefungua njia mpya na bunifu za kuhamasisha na kuandikisha wanachama. Hili liliongezeka sana wakati wa janga la UVIKO-19, ambapo vyama vilibuni njia za kidigitali za kuwasiliana na wanachama, kufanya mikutano, kusaidia wafanyakazi waliokumbwa na matatizo, na kuendelea na uandikishaji wa wanachama wapya. Gloria Kente wa SADSAWU, Afrika Kusini, anaeleza:

"Haikuwa rahisi kuhamasisha wafanyakazi wa majumbani wakati wa UVIKO 19. Hata hivyo, matumizi ya simu janja yalisaidia sana kuwafikia wanachama. Wahamasishaji walitengeneza vipeperushi vinavyoeleza kuhusu SADSAWU na sababu za kujiunga. Walipiga picha za vipeperushi hivyo na kuzituma kwa wajumbe wa kamati wanaoishi na wafanyakazi wa majumbani katika jamii."

Whatsapp ni chombo chenye nguvu sana cha kutuma habari kuhusu chama na shughuli zake. Pia ni muhimu kwa kuhamasisha. Wanachama hupokea jumbe za Whatsapp na kuzituma kwa wafanyakazi wengine wa majumbani wakiwahimiza kujiunga.

"Tunatumia Whatsapp. Wafanyakazi wengi wa majumbani wanapata huduma hii na ni rafiki kwa watumiaji. Tunaitumia kuhamasisha. Tunatuma taarifa za chama, masuala muhimu kwa wafanyakazi wa majumbani, kuongeza uelewa wa haki zao na kampeni zetu. Pia tunachapisha taarifa za ndani, kikanda na kimataifa kuhusu IDWF. Hili ni muhimu kwa vile wanajua kuwa hawajatengwa katika mapambano yao na kwamba wana sauti ya kimataifa." (Toindepi Dhure, ZDAWU, Zimbabwe)

Wakati wa kufungwa kwa mipaka ya nchi na vikwazo vya UVIKO-19, vyama vya wafanyakazi pia vilijifunza kutumia simu janja kama zana ya kufanya mikutano. SADSAWU, kwa mfano, inatumia Google Meet kufanya mikutano na viongozi kote Afrika Kusini.

*Kwa kutumia mitandao ya kijamii*

Matumizi ya simu janja yameongeza uwepo wao kwenye mitandao ya kijamii. Debora Mwageni kutoka CHODAWU, Tanzania, anabainisha:

"Tuna Facebook na Instagram. Ili kuandikisha wanachama wapya tunachapisha shughuli zetu zote kwa wale ambao ni sehemu ya chama. Wanapitisha habari au kuonyesha wengine. Wafanyakazi wa ndani pia huchapisha matatizo yao na kuuliza, "Tunaweza kufanya nini?" Tunajibu na kuwapa taarifa".

SADSAWU pia hutumia Tik Tock kushiriki video zilizotengenezwa na wahamasishaji na viongozi.

Inafurahisha kwamba viongozi wengi wanaripoti kwamba waajiri wanapata habari kuhusu chama kupitia Facebook.

"Tunachapisha kwenye mitandao ya kijamii siku za matukio kama vile Mei Mosi. Tunazungumza kuhusu manufaa ya kujiunga na chama. Waajiri pia wanaweza kuona na kujifunza kutokana na hili. " (Joan Gloria, KUDHEI- HA, Kenya)

Waajiri pia hupata mawasiliano ya chama kwenye Facebook na baadhi huwasiliana na Chama kwa ushauri.

### 6. Kushirikisha wafanya maamuzi

Wafanyakazi wa majumbani wanataka kuona kuwa chama chao kinafanya kazi kwa ufanisi na kinaweza kuleta mabadiliko ya kweli. Kuwashirikisha viongozi wa serikali na waajiri kupitia majadiliano na hasa kupitia mazungumzo ya moja kwa moja ni mkakati wenye nguvu sana. Wafanyakazi wanapoona kuwa serikali au waajiri wanawasikiliza viongozi wa chama, hujivunia kuwa sehemu ya chama hicho na huamini kuwa chama kinawatetea kwa vitendo. Hali hii huwapa sababu ya kuwahamasisha wafanyakazi wengine wa majumbani kujiunga.

Vyama vingi vya wafanyakazi wa majumbani tayari vimejenga uhusiano chanya na maafisa wa serikali au idara husika:

"Wanatusaidia kwenye kampeni za uhamasishaji, kwa mfano kupitia mtandao, televisheni na mikutano ya kanda. Wanatuhusisha kwenye majadiliano kuhusu m ishahara ya kima cha chini. Wanatusaidia kwenye kesi. Hawafanyi mazungumzo na w aajiri bila wawakilishi wa chama." (Nellie Kahua, NDAWU, Namibia)

Katika baadhi ya nchi, vyama vya wafanyakazi wa sekta nyingine vinavyohusiana pia husaidia v yama vya wafanyakazi wa majumbani kufikia s erikali au kuwapatia msaada wa kiufundi. "Chama cha wafanyakazi tulichojishirikisha n acho kinatusaidia," notes Asmaou Bah.

V yama vingi vinafanikiwa kukuza uanachama k wa kutumia mbinu mchanganyiko. Mfano mzuri wa hilo unapatikana nchini Msumbiji.

## BOKSI 07

## HADITHI KUTOKA MSUMBIJI

*Kutumia mikakati mbalimbali: Mfanyakazi mwenye kujiamini*

Jina langu ni Gisela Cossa, mimi ni mama mwenye mtoto mmoja. Nimekuwa nikifanya kazi kama mfanyakazi wa majumbani tangu mwaka 2012. Nilijiunga na chama cha SINED mwaka 2017 baada ya kundi la wafanyakazi wa majumbani kupita karibu na mahali nilipokua nafanya kazi. Niliamua kujiunga nao. SINED ni chama cha wafanyakazi wa majumbani nchini Msumbiji. Kina wanachama 14,667 wakiwemo wanaume 1,732 na wanawake 12,935. Kina matawi kumi yaliyosambaa katika mikoa ya Maputo, Gaza, Inhambane, Sofala, Manica, Zambézia, Tete, Nampula, Niassa, na Cabo Delgado. Mwaka 2021, tulifanikiwa kuwaandikisha wanachama wapya 800 kutoka maeneo mbalimbali nchini. Kampeni hii ilileta athari kubwa jijini Maputo, ambako takriban wafanyakazi wa majumbani 312 walifukuzwa kazi kutokana na athari za janga la UVIKO 19. SINED liliweza kutoa msaada wa kisheria kwa wafanyakazi 19 kati yao. Baada ya kujiunga na chama, nilianza kushiriki mikutano ya wanachama iliyokuwa ikiandaliwa na SINED kila Jumapili katika Kituo cha Vyama vya Wafanyakazi (OTM). Katika mikutano hiyo, nilichaguliwa kuwa kiongozi wa kitengo cha chama na mratibu wa wafanyakazi wa majumbani katika eneo la Casas Brancas, kwenye mtaa wa Polana Caniço, pembezoni mwa Jiji la Maputo.

Nataka kutumia fursa hii kueleza kwa kifupi uzoefu wangu wa kushiriki katika kampeni ya uandikishaji wa wanachama wa chama chetu. Kila siku, isipokuwa Jumamosi na Jumapili, huamka saa 10 alfajiri, na kuondoka nyumbani saa 11:20 alfajiri

kwenda kazini, ambako hufika saa 1:00 asubuhi. Njia nawaeleyea kila mfanyakazi wa majumbani ntakae kutana nae kuhusu chama Chama.

Katika siku za Jumamosi na Jumapili, ninaungana na viongozi wenzangu wa wafanyakazi wa majumbani. Tunazunguka jiji la Maputo, tukifanya kampeni ya nyumba kwa nyumba, katika majengo au nyumba, masoko, viwanja, maduka na masupermarket. Tunagawanya vifaa vya kampeni kama vile vipeperushi. Tunatumia pia njia hii ya kampeni kuwafikia wanachama wapya katika miji mikuu ya mikoa ambako SINED imeanzishwa.


Tunapotaka kuanzisha tawi jipya, jambo la kwanza tunalofanya ni kuwasiliana na viongozi wa mitaa ya eneo husika. Kisha tunajaribu kuwatambua wafanyakazi wa majumbani wanaofanya kazi au kuishi katika maeneo hayo ya makazi.

Baada ya kuwahamasisha angalau wafanyakazi wa majumbani 30, tunaandaa kikao cha kuwaeleza umuhimu wa kujiunga na chama cha wafanyakazi. Tunazungumza kuhusu sharia, haki na faida za kuwa mwanachama. Kwa kawaida katika mikutano hii, wafanyakazi wa majumbani huchagua kwa kupiga kura kiongozi wa kamati ya chama atakayewawakilisha.

Ninashiriki pia katika vipindi vya televisheni na redio, ambapo ninazungumzia kuhusu kanuni za kazi za wafanyakazi wa majumbani, unyanyasaji wa kingono, ukatili wa kijinsia, Mikataba ya ILO namba 189 na 190, hifadhi ya jamii na masuala mengine muhimu kwa wafanyakazi wa majumbani. Hii huongeza uelewa na kuwavutia wafanyakazi wa majumbani kujiunga na chama. Matumizi ya Facebook, WhatsApp na Instagram pia yamekuwa msaada mkubwa kuwajulisha wanachama kuhusu chama na umuhimu wa kujiunga.

Kwa kumalizia, napenda kusema kuwa najivunia kuwa mfanyakazi wa majumbani kwa sababu napenda kazi ninayofanya, na hiyo inachangia sana mafanikio ya kampeni na kazi zetu. Siri nyingine ya mafanikio ya kampeni zetu za kuandikisha wanachama wapya ni mawasiliano mazuri tunapozungumza na wanachama. Ujumbe unaotaka kuwafikishia lazima uwe wazi, rahisi na unaoeleweka kwa urahisi.

> Vyama vyetu vingi vya wafanyakazi vimeweza kuendeleza uhusiano mzuri na maafisa/taasisi husika za serikali.



SURA YA 05

# KUMBUKUMBU ENDELEVU KATIKA KUANDIKISHA

Ni muhimu sana kwa Chama cha wafanyakazi kuhakikisha kwamba wanachama wapya wanajaza fomu ya maombi au usajili, na chama kinatoa kadi za uanachama (au kitu kinachofanana). Tunapaswa kuwajua wanachama wetu ni kina nani na namna ya kuwafikia. Tunapaswa kuwa na taarifa za kisasa kuhusu hali yao ya ulipaji wa ada ya uanachama. Vyama vingi vya wafanyakazi vinaripoti kuwa vinatunza kumbukumbu. "Kutunza kumbukumbu ni utamaduni wa vyama," anasema Toindepi Dhure (ZDAWU, Zimbabwe). Baadhi ya vyama huweka kumbukumbu kwa mikono kwenye vitabu; vingine hutumia kompyuta kwa kutumia Excel, na vingine vina mifumo ya kisasa ya kompyuta kwa ajili ya kumbukumbu. Ni muhimu pia kwa wanachama kujua kuwa wamesajiliwa rasmi na chama, na kuwa na uthibitisho wa uanachama ambao wanaweza kuonyesha na kujivunia. Hili husaidia kujenga utambulisho kama mfanyakazi wa majumbani, na pia hujenga mshikamano na wafanyakazi wengine wa majumbani. Kuwa na kumbukumbu ni muhimu sana kwa ajili ya kuwaendeleza wanachama wetu: tunaweza kuwasiliana nao, kuwaalika kushiriki katika shughuli, kuripoti mafanikio ya shughuli zetu, na kadhalika. Hii pia ni muhimu kwa uendelevu wa chama.

Nellie Kahua kutoka NDAWU anasimulia hadithi ya jinsi chama hicho, kwa msaada kutoka shirikisho la vyama vya wafanyakazi, kilivyotambulisha kadi ya kisasa ya uanachama, ambayo pia inashughulikia hitaji kubwa la wafanyakazi wa majumbani na inaunganishwa na mfumo sahihi wa kuweka kumbukumbu. Hili linasaidia kuvutia wanachama wapya huku likiwawezesha pia wanachama waliopo kuendelea kubaki kwenye chama. Pia linarahisisha ukusanyaji wa ada za uanachama.



BOKSI

# HADITHI KUTOKA NAMIBIA

08

## *Kadi maalum ya uanachama*

Jina langu ni Nellie Dina Kahua. Mimi ni Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Majumbani na Sekta nyinginezo cha Namibia (NDAWU). Chama chetu kilianzishwa mwaka 2015. Tuna wanachama kati ya 3,000 hadi 3,700.

Mfanyakazi wa majumbani anapojiunga na chama chetu hujaza fomu ya uanachama na kulipa ada ya uanachama. Wanachama hupokea kadi ya uanachama. Hapo awali tulikuwa tunatumia kadi za karatasi. Lakini mambo yamebadilika, sasa tunatoa kadi ya plastiki ya uanachama ambayo pia ni kadi ya Visa. Kwenye kadi hiyo kuna jina la chama, nembo ya chama, na namba ya uanachama wa mfanyakazi.

Kupitia kadi hii ya Visa, mwanachama anaweza kuweka akiba, kupokea mshahara wake, kununua umeme au vocha ya simu, kutoa pesa kwenye ATM, na kulipa ada ya uanachama. Kadi haina muda wa kuisha, hivyo mfanyakazi wa majumbani anaweza kuendelea kuitumia hata baada ya kustaafu, japokuwa anafutwa kwenye mfumo wetu wa taarifa na haendelei kulipa ada ya uanachama.

**Kwa nini na vipi hili lilifanyika?**

Tulitambua changamoto walizokuwa wanakutana nazo wafanyakazi wa majumbani. Tulijiuliza tunawezaje kuwasaidia wafanyakazi wa majumbani kutunza fedha zao. Hawakuwa na akaunti za benki kwa sababu kufungua akaunti kunahitaji kiwango cha chini cha kufungulia, ambacho wengi wao hawakuwa nacho. Kadi hii imetatua tatizo hilo.

Mpango huu ulijadiliwa na shirikisho letu, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Namibia (NUNW). Shirikisho lilianzisha kitengo cha biashara cha vyama ambapo vyama vikubwa vinawekeza fedha kwa mipango ya baadaye. Kwa msaada wa taasisi yetu ya utafiti, walikuja na wazo bora la kusaidia wanachama wa NDAWU kuondokana na changamoto ya huduma za kibenki. Walifanya mazungumzo na benki ili kuunganisha kadi ya uanachama/Visa na mfumo wa kibenki. Mfumo huu unafanya kazi vizuri na unatusaidia kuwahifadhi wanachama wetu kwa sababu unakidhi moja ya mahitaji yao halisi.

**Kutunza kumbukumbu**

Mpango huu pia unasaidia chama kuweka kumbukumbu bora. Tuna mfumo wa data ambapo tunahifadhi taarifa za wanachama wapya wote. Mfumo unaonyesha ni nani amelipa ada za chama na nani hajalipa. Hili hufanya iwe rahisi kuwakumbusha wanachama kwa kutuma ujumbe mfupi au kuwapigia simu. Viongozi wawili wanasimamia mfumo huu.

# 06 MAFUNZO KUTOKANA NA UZOEFU WETU




*Je, ni funzo gani tunaweza kujifunza kutokana na uzoefu huu wote wa kukuza vyama vyetu? Hapa kuna mambo muhimu ya **"Kufanya" na "Kuepuka"** ambayo tunapaswa kuyakumbuka tunapowahamasisha wanachama wapya na kuendelea kuwatunza waliopo. Unaweza pia kuongeza mengine.*

BOKSI

# HADITHI KUTOKA GUINEA

09

## *Mambo ya kufanya na kutofanya katika uhamasishaji*

**FANYA HAYA:**

- Panga vizuri
- Elewa na urekebishe mikakati yako kulingana na mazingira ya eneo husika
- Sikiliza kwa makini wasiwasi na matatizo ya wafanyakazi wa majumbani.
- Mfanye mfanyakazi ajisikie kuwa matatizo yake ni ya muhimu
- Jitahidi kadri ya uwezo wako kujibu maswali na kuondoa mashaka ya wafanyakazi
- Tafuta suluhisho la matatizo na toa ushauri
- Wasiliana kwa njia fupi, rahisi na inayoeleweka kwa urahisi
- Tumia lugha wanayoielewa vizuri na wanayoijua
- Hakikisha unao muda wa kutosha, usionekane una haraka
- Hamasisha wafanyakazi wa majumbani wenyewe kushiriki katika uandikishaji na watambue kazi zao vizuri
- Tumia vifaa/mitandao vinavyofaa kuwavutia na kuwapa hamasa wafanyakazi
- Panga utaratibu wa kufuatilia waliojiunga
- Shirikiana na vyama vya wafanyakazi na washirika wengine
- Tumia mikakati mbalimbali, ikiwemo kukutana ana kwa ana na teknolojia mpya
- Wafanye wafanyakazi wa majumbani wajione kuwa sehemu ya harakati ya kimataifa kwa kuwajulisha kuhusu IDWF

**USIFANYE HAYA:**

- Usiahidi kitu ambacho huwezi kutimiza
- Usipange tarehe au ahadi halafu usijitokeze.
- Usipuuze matatizo na wasiwasi wa wafanyakazi.
- Usikwepe kujibu maswali magumu, kama vile kuhusu michango ya chama
- Usizungumze sana au kuhubiri kama unaelekeza darasani
- Usiwe na haraka au kukosa uvumilivu

SURA YA



07



# NINI KINACHOFUATA?

*Kama tulivyoona, kuandikisha wanachama wapya pekee hakutoshi kukuza na kudumisha chama imara cha wafanyakazi wa majumbani. Tunapaswa kukifanya kuwa sauti yenye nguvu kwa wafanyakazi wa majumbani katika nchi zetu, barani Afrika na duniani kote kupitia IDWF. Tunawezaje kufanikisha hili? Hapa kuna baadhi ya miongozo.*



BOKSI

10

# CHAMA IMARA

## *Kudumisha Chama imara: Miongozo*

Kua imara, mbunifu na mwajibikaji

- Endelea kuandikisha wanachama kutoka maeneo mapya na ya zamani
- Hakikisha wanachama waliopo wanajihusisha na kushiriki kikamilifu
- Hamasisha na endesha kampeni kuhusu masuala na madai ya wafanyakazi wa majumbani
- Kila mara shughulikia matatizo na kesi binafsi za wanachama
- Onyesha nguvu ya chama kwa kujadiliana au kufanya mazungumzo na serikali na waajiri
- Wajengee wanachama uwezo kwa kutoa elimu na mafunzo kuhusu masuala ya chama, haki zao na ujuzi muhimu
- Hakikisha mawasiliano mazuri na ya mara kwa mara kati ya viongozi na wanachama

Kuwa na Miundo ya Kidemokrasia Inayofanya Kazi Vizuri


- Fuata katiba ya chama
- Fanya mikutano ya mara kwa mara na yenye ushiriki mzuri
- Chukua maamuzi kwa kushirikisha wafanyakazi na kufuata maelekezo yao
- Toa taarifa za kazi za chama kwa wakati na kwa uwazi
- Fanya chaguzi kwa mujibu wa katiba mara kwa mara
- Kuwa na viongozi waaminifu, wawajibikaji na wenye kujitolea
- Simamia vizuri fedha za chama kwa uwazi na uwajibikaji
- Hifadhi kumbukumbu muhimu kwa usahihi



# ...

# HITIMISHO

Maneno ya mwisho katika kijarida chetu yanatoka kwa mratibu wa kanda ya Afrika, Vicky Kanyoka.



## 08

"Lengo la Kwanza la Kimkakati la IDWF ni maendeleo ya shirikisho, ambalo linajumuisha shughuli za uandikishaji na uhamasishaji wa wanachama. Hii ina maana kwamba nguvu ya chama chochote cha wafanyakazi inategemea wanachama. Wanachama ndio uti wa mgongo wa chama chochote na hivyo ndivyo ilivyo kwa vyama vya wafanyakazi wa majumbani. Kupitia wanachama ndipo vyama hupata nguvu, umoja na mshikamano. Wanachama wetu barani Afrika wamekuwa wakifanya kazi kwa bidii kuhamasisha, kuelimisha, kuandaa na kuandikisha wanachama tangu mwaka 2009. Wanachama hao wamekuwa wakiongezeka kwa asilimia kati ya 50% hadi 100% kila mwaka. Kupitia kazi hii, wamepata uzoefu mbalimbali wa jinsi ya kufanikisha uandikishaji huo.

Hata hivyo kupitia kitabu hiki tunajifunza kuwa hakuna njia moja ya kuhamasisha na kuandikisha wafanyakazi wa majumbani. Viongozi wa chama wamekuwa wabunifu sana na kutumia mbinu mbalimbali katika uandikishaji wa wanachama kwenye vyama vyao jambo ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uanachama na uwezo wa kulipa ada ya uanachama kwa IDWF.




Ni matarajio ya viongozi wa IDWF kwamba kijarida hiki kitakuwa ni miongoni mwa rasilimali muhimu zitakazowasaidia wanachama, viongozi na wadau kujifunza zaidi kuhusu mchakato wa kuhamasisha na kuandikisha wanachama na jinsi tunavyoutekeleza hapa barani Afrika."

Tunawashukuru viongozi wote, wanachama wa vyama/mashirika ya wafanyakazi wa majumbani barani Afrika kwa mchango wao mzuri uliowezesha kupatikana kwa kijarida hiki."

**Hamasisha kwa ajili ya Nguvu! Hamasisha kwa ajili ya Umoja!!**

**Hamasisha kwa ajili ya Mshikamano!**

> Ni kupitia uanachama ndipo vyama vya wafanyakazi hupata nguvu, umoja na mshikamano

# TIMU YA IDWF AFRIKA



**ASMAOU BAH**
MJUMBE WA KAMATI TENDAJI



**ESSI KOTOR**
AFISA MIPANGO



**VICKY KANYOKA**
MRATIBU WA KANDA



**DEOGRASIA VULUWA**
AFISA MIPANGO



# BAADHI YA RASLIMALI MUHIMU

## *JUU YA KUANDAA*

StreetNet na WIEGO, "Kupanga katika Uchumi Usio Rasmi. Vitabu vya Nyenzo-rejea kwa Waandaaji", mfululizo wa vijitabu 6 (vinapatikana katika Kiingereza, Kifaransa, Kireno)

1. Kuhamasisha Wafanyakazi wa sekta hisiyo Rasmi katika Mashirika ya Wafanyakazi ya Kidemokrasia
2. Kujenga na Kudumisha Shirika la Kidemokrasia la Wafanyakazi Wasio Rasmi
3. Kushughulikia Matatizo ya siku kwa siku ya Wafanyakazi Wasio Rasmi
4. Majadiliano ya Pamoja kwa Wafanyakazi Wasio Rasmi
5. Kushughulikia Migogoro kati ya Wafanyakazi Wasio Rasmi na wale walio Madarakani
6. Hatua za Pamoja kwa Wafanyakazi Wasio Rasmi

https://www.wiego.org/worker-education-advocacy-materials

ITUC-CSI, "Decent work, decent life for domestic workers"

https://www.ituc-csi.org/IMG/pdf/ITUC_dwd_AnglaisWEB.pdf

IDWF and NDWA, International Domestic Workers Day, Outreach and Visibility Campaign. A Toolkit

https://idwfed.org/wp-content/uploads/2022/08/international_domestic_workers_day_outreach_and_visibility_campaign_en.pdf

Burke,Geronima, Martina,Thomas,Wall," Education for Changing Unions."

## *KATIKA MKATABA NA.189*

IDWF na WIEGO. "Zana yako kuhusu Mkataba wa ILO Na. 189. Mkataba wa Wafanyakazi wa Majumbani (Kanda ya Afrika)

https://www.wiego.org/sites/default/files/resources/files/Domestic_Worker_Toolkit_WIEGO_IDWF_Web.pdf


## *JUU YA MAZOEA BORA*

IDWF na ILO. Kazi nzuri kwa wafanyakazi wa majumbani. Mbinu nane nzuri kutoka Asia

https://idwfed.org/wp-content/uploads/2022/08/eight_good_practices_from_asia_en.pdf

*Kushiriki mbinu zetu bora za kuajiri barani Afrika*

# “HAMASISHA, HAMASISHA, HAMASISHA. JINSI GANI TUNAFANYA!”




**Shirikisho la Kimataifa la Wafanyakazi wa Majumbani**

www.idwfed.org